THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

**021**

# KISWAHILI
## (Kwa Watahiniwa Walioko na Wasioko Shuleni)

**Muda: Saa 3** *Alhamisi*, **Oktoba 13, 2005 Asubuhi.**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali yote katika sehemu A, B, C na D na maswali **mawili (2)** kutoka sehemu E.
3. Zingatia maagizo ya kila sehemu na ya kila swali.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
5. Mashine za hesabu za elektroniki **haziruhusiwi** kwenye chumba cha mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

CPB

Karatasi hii ina kurasa *6* zenye maandishi.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 10)

**Jibu maswali yote katika sehemu hii.**

## UFAHAMU

1. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika kijitabu chako cha kujibia.

Iwapo hali iliyopo sasa barani Afrika haitabadilika, Ukombozi wa Mwafrika wa kujitoa katika madhila makubwa yasiyosemeka utakuwa ni ndoto tupu. Utengano unaotokana na ukabila, usomi na hata utaifa ambao umezagaa katika bara hili, ubadhirifu wa mali za umma, ulaji rushwa, uhujumu na udikteta, ubinafsi, uongo, unafiki, ushirikina, utaifa, upendeleo na uchoyo, uzembe, umalaya, usaliti na uovu mwingine mwingi tunaoishi nao Afrika. Utamaduni wa Mwafrika wa kupendana na kushikamana, wa heshima na adabu kwa mkubwa na mdogo, wa utu na huruma, wa kazi na uaminifu unadidimia.

Wakati wa uhai wake mzalendo wa bara hili Kwame Nkrumah alipigania sana umoja miongoni mwa Waafrika kama wa jamii moja na taifa moja. Aliwakumbusha Waafrika mfano wa Marekani jinsi wanamapinduzi katika jamii hiyo walivyokuwa na welewa mkubwa wa haja ya umoja miongoni mwa wananchi. Hivyo walipigana vita vya wenyewe kwa wenyewe ili kuulinda umoja wa kisiasa wa taifa lao ambao ulikuwa ukitingishwa na baadhi ya wasiopenda maendeleo. Alikumbusha pia umoja wa Urusi, jinsi harakati za kuleta umoja wa bara hilo na juhudi za kurejesha hadhi ya taifa huru la Warusi zilizofanywa na majimbo ya shirikisho zilivyoleta mabadiliko ambayo yameiinua jamii duni na kufikia upeo wa jamii yenye nguvu sana katika kipindi kifupi sana. Kutokana na mifano ya Marekani na Ulaya, ni wazi kuwa sisi tuliomo Afrika tunazo raslimali na uwezo wa kuanzisha jamii ambayo tuna hamu nayo kuijenga.

Bara la Afrika ni la pili kwa ukubwa duniani. Utajiri wa asili uliomo Afrika unakadiriwa kuwa unazidi wa bara lingine lolote ulimwenguni. Ili Waafrika tunufaike na raslimali tuliyonayo na uwezo tulionao, tuweze kupata mafanikio ya amani na maisha bora, yatubidi tuunganishe juhudi zetu, raslimali zetu, ujuzi wetu na shabaha zetu.

Kwa shabaha ya kulinganisha yaliyotokea Ulaya, ambayo nasi Waafrika yalituathiri vikubwa, yawe fundisho kubwa kwetu sote. Kwa kukazania utaifa wa nchi moja, vita vimepiganwa kwa karne kadhaa; vita ambavyo vilihatarisha amani na kuangamiza maisha ya mamilioni ya watu, wakiwemo Waafrika, na kuleta hali ya wasiwasi. Sababu ya kutokea hali hiyo ni kwamba Ulaya huko nyuma haikujenga misingi imara ya umoja wa kisiasa na uelewano.

Tuligawanywa ili tutawaliwe vyema na wakoloni. Kwa kudumisha lugha ngeni tumeendelea kudunisha utamaduni wa Mwafrika na tumekubali kugawanywa kwa kufuatana na lugha ngeni. Lakini tukumbuke kuwa Mwafrika azungumzaye Kiingereza, Kifaransa au Kireno kamwe hatakuwa Mwingereza, Mfaransa au Mreno.

Kwetu sisi Afrika na visiwa vyake ni Afrika moja. Tunapinga wazo lolote la kugawanywa kutoka Tangier au Cairo huko Kaskazini hadi Cape Ghardafui huko Mashariki hadi visiwa vya Cape Verde huko Magharibi. Afrika ni moja haijagawanyika. (Nkrumah 1973 uk. 22 -- 23).

Tumejifunza kutoka kwenye mataifa yaliyoendelea kwamba maendeleo yanapatikana kwa harakati za kihistoria zenye mfuatano wa mapinduzi ya siasa, utamaduni na uchumi.

Nchi zenye viwanda huko nyuma hazikukazania vitega uchumi bali zilikazania maendeleo ya kisiasa na utamaduni. Huko Marekani, Ulaya Magharibi na hivi karibuni Japan, usalama wa kisiasa ulihimizwa kwanza.

Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

**MASWALI**

(i) Kichwa cha habari kinachofaa kwa habari hii ni

A Ukombozi wa Mwafrika
B Kuungana kwa Marekani na Ulaya
C Waingereza, Wafaransa na Wareno
D Msimamo wa Nkrumah kuhusu Marekani
E Mapinduzi Afrika.

(ii) Kwame Nkrumah alikuwa akitaka pawepo na

A utamaduni wa Mwafrika
B umoja wa Afrika
C mapinduzi Afrika
D utawala bora wa nchi za Afrika
E mzalendo wa Afrika.

(iii) Mzalendo wa Bara hili maana yake halisi ni

A Kwame Nkrumah
B Waafrika wote wenye mapenzi ya dhati ya Bara la Afrika
C Mwafrika mwenye mapenzi ya dhati kwa Bara la Afrika
D mpenda mapinduzi
E mpinga mapinduzi.

(iv) Ukabila, usomi na utaifa katika Afrika umesababishwa na

A usaliti na uonevu
B udikteta
C ushirikina
D utengano
E ubinafsi.

(v) Jamii iliyokuwa na uelewa mkubwa wa umoja ni

A Waafrika
B Warusi
C Wafaransa
D Waingereza
E Wamarekani.

(vi) Utajiri wa Bara la Afrika ni wa

A kwanza duniani
B pili duniani
C tatu duniani
D wachache
E wote waliomo Afrika.

(vii) Ili Waafrika tunufaike na raslimali zetu yatubidi

A tusome sana tupate elimu ya kutosha
B tuunganishe juhudi, raslimali, ujuzi na shabaha zetu
C tufanye mapinduzi kama yale ya Marekani na Ulaya
D tufanye vita vya wenyewe kwa wenyewe ili tuungane
E tuziuze kwa bei nzuri.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

(viii) Vita vilipiganwa kwa karne nyingi kwa sababu ya

- A raslimali za Afrika
- B uchoyo, unafiki, ubinafsi, upendeleo na kadhalika
- C kukazania utaifa wa nchi moja
- D kuleta umoja wa nchi za Marekani na Ulaya
- E fundisho kubwa kwetu sote.

(ix) Tuligawanywa ili tutawaliwe vyema na wakoloni kwa

- A kudumisha lugha ngeni
- B kudunisha utamaduni wa Mwafrika
- C kuzungumza Kiingereza, Kifaransa na Kiafrika
- D kufuatana na lugha ngeni
- E kununuliwa viongozi wetu na wakoloni.

(x) Nchi zenye viwanda huko nyuma zilikazania

- A vitega uchumi
- B maendeleo ya uchumi
- C utamaduni na vitega uchumi
- D siasa, uchumi na utamaduni
- E maendeleo ya kisiasa na utamaduni.

2. Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha andika ufupisho wa maneno **40**.

Kazi ya ukuli ilikuwa ngumu, ikamchosha kabisa Rashidi, lakini alikuwa hana la kufanya, ila kuendelea nayo ili aweze kupata maisha. Pesa zenyewe zilikuwa hazitoshi, matumizi yake yalizidi; madeni yalimtopea. Mbali ya kidani cha mama yake alichokiweka rehani, alikuwa anadaiwa na washihiri chungu nzima wenye maduka. Rashidi hakuweza kufanya jambo lolote la anasa, na ile sinema ambayo kila siku alikuwa na hamu ya kwenda kuiona, alikuwa anakwenda kwa mdomo tu.

Rashidi alisimama kando ya pwani ya Gulioni kwa muda akifikiri hata mwisho, alinong'ona peke yake, "Ama! Haya kama yataweza kubadilika, itakuwa kheri kubwa". Kisha taratibu alijiburura kuelekea kibaruani.

## SEHEMU B (alama 20)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

## UTUMIZI WA LUGHA

3. Chunguza kwa makini orodha **A** na **B** kisha eleza maana ya vifungu vya maneno katika orodha **A** kwa kutumia orodha **B**. Andika herufi ya jibu kando ya namba ya swali.

| ORODHA A | | ORODHA B | |
|---|---|---|---|
| (i) | Malaika, shetani, mzimu | A | Nomino za mguso |
| (ii) | Hucheza | B | Neno lenye silabi moja |
| (iii) | Juzi asubuhi | C | Kirai kielezi |
| (iv) | Mwalimu wetu anakuja | D | Njeo ya wakati uliopo |
| (v) | Nywa | E | Nomino za dhahania |
| | | F | Kirai nomino |
| | | G | Kivumishi kimilikishi |
| | | H | Njeo ya wakati wa mazoea |
| | | I | Kivumishi cha sehemu |
| | | J | Kiambishi. |



Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

4. Andika sentensi zifuatazo kwa usahihi.

(a) Nimekodisha lori linipelekee vifaa vya ujenzi.

(b) Ng'ombe wangu ni mjamzito wa miezi nane.

(c) Nilikuja kwa nauli yangu mwenyewe.

(d) "Ulikuwa wapi?" "Nilitoka nje nilikuwa na mgeni."

(e) Baba yangu ana ugonjwa kisukari.

5. (a) Taja tofauti **tano (5)** zilizoko baina ya barua ya kirafiki na barua ya kikazi.

(b) Andika barua kwa mlezi/mzazi wako ili umweleze siku utakayowasili nyumbani baada ya kumaliza Mtihani wako wa Kidato cha Nne. Jina lako liwe Sondo Msondoka; jina la mlezi/mzazi wako liwe Msondoka Maringo wa kitongoji cha Metameta. Anuani yako iwe S.L.P. 40, Mabuchani.

## SEHEMU C (alama 20)

Jibu maswali yote katika sehemu hii.

### SARUFI

6. Taja aina za maneno yaliyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

(a) Juma ndiye msomaji mzuri.

(b) Kucheza tunakupenda lakini kunapoteza muda.

(c) Chumbani kumepambika.

(d) Nenda chumbani ukapumzike.

7. "Maana na mpangilio wa maneno katika sentensi ni vigezo muhimu vya kumsaidia mtu kutambua aina za vielezi (E)." Tumia mbinu hizo kueleza aina **nne (4)** za vielezi (E).

8. (a) Nini maana ya mzizi wa neno?

(b) Onesha mizizi ya maneno yafuatayo:

(i) Salisha

(ii) Anakunywa

(iii) Onyesha

(iv) Onesha.

9. Onesha idadi ya silabi za maneno yaliyopigiwa mstari:

(a) Baba amefuga mbwa mkali.

(b) Yai la mbuni ni kubwa kuliko la kuku.

(c) Haya ni maji ya kunywa tu.

(d) Mbuni ukiota unaishi miaka mingi.

(e) Magonjwa mengi husababishwa na nzi.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU D (alama 10)

Jibu swali la **kumi (10)**.

## HISTORIA YA LUGHA

10. Fafanua kwa kifupi taasisi **tano (5)** zinazotumiwa kukuza na kueneza Kiswahili Tanzania.

## SEHEMU E (alama 40)

Jibu maswali **mawili (2)** kutoka sehemu hii. Swali la **13** ni la lazima.

## FASIHI

## ORODHA YA VITABU

### USHAIRI

| | | |
|---|---|---|
| DIWANI YA MLOKA | - | C. MLOKA |
| MASHAIRI YA CHEKACHEKA | - | T. A. MVUNGI |
| MALENGA WAPYA | - | TAKILUKI |

### RIWAYA

| | | |
|---|---|---|
| KUSADIKIKA | - | S. ROBERT |
| WATOTO WA MAMA NTILIE | - | E. MBOGO |
| KIU YA HAKI | - | Z. M. MWANGA |

### TAMTHILIYA

| | | |
|---|---|---|
| NGOSWE – PENZI KITOVU CHA UZEMBE | - | E. SEMZABA |
| MFALME JUHA | - | F. M. TOPAN |
| KILIO CHETU | - | MEDICAL AID FOUNDATION |

11. Ni mambo gani ya kimsingi katika Fasihi Simulizi yanayodhihirisha uhai na uhalisi wake?

12. "Dhana ya mapenzi inajitokeza kwa ukweli na uongo". Fafanua kauli hiyo ukitumia riwaya mbili kati ya hizo zilizoorodheshwa hapo juu.

13. Taswira ni kipengele muhimu katika kuipamba lugha ya ushairi na kufikisha ujumbe kwa hadhira. Onesha ukweli huo kwa kutumia vitabu viwili vya ushairi kati ya vilivyoorodheshwa hapo juu.

14. "Wahusika katika tamthiliya hupambanishwa na mwandishi kwa nia ya kuibua matatizo katika jamii na kuyatolea utatuzi." Dhihirisha kauli hiyo kwa kutumia tamthiliya mbili kati ya hizo zilizoorodheshwa hapo juu.



Find this and other free resources at:
https://maktaba.tetea.org